

Jinsi Samyog Ana-vyomfuata Yesu

Nchini Nepal, Wakristo ni wacha-che. Watu wengi hawafahamu mengi kuhusu Yesu Kristo. Samyog hupenda kuwaambia wengine kuhusu Yesu.

Wakati fulani, shule ya Samyog ilikuwa na sherehe za Krismasi ili kuwasaidia wanafunzi wajifunze kuhusu siku za mapumziko ulimwengu kote. Samyog alishiriki kwa-mba yeye ni Mkristo. Alijibu maswali ya walimu na wanafunzi kuhusu Yesu.

"Ninataka kumfuata Yesu maisha yangu yote," Samyog alisema. ●

VIELELEZO NA AARON CUSHLEY

Kuhusu Samyog

MIAKA: 9

KUTOKA: Jimbo la Bagmati, Nepal

LUGHA: Kinepali, Kingereza

MALENGO NA NDOTO: 1) Kuwa rubani. 2) Kumfuata Yesu Kristo. 3) Kumwita mtoto wake wa kwanza wa kiume "Sreejal," ambayo humaanisha utakaso.

FAMILIA: Samyog, Aama (Mama), Buba (Baba), na didis wawili (dada wakubwa)

KUTANA NA SAMYOG!



Mambo ayapendayo Samyog

HADITHI KUHUSU YESU:
wakati alipokufa kwa ajili yetu kwa sababu anatupenda

WIMBO WA MSINGI:
"Follow the Prophet"
(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 110-11)




MAHALI:
Sebule ya nyumbani kwao

VYAKULA:
Keki na kukhura (kuku)



RANGI:
Machungwa na samawati

MASOMO SHULENI:
Sayansi na hisabati



Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!

Kuna njia nyingi za kumfuata Yesu. Je, ni kwa namna gani wewe unamfuata Yeye? Andika na utuelezee!

